COUNTY MOCK EXAMS-STD 8
2016

KISWAHILI PAPER

Coordinated by KENPRO,
Macjo Arcade, 4th Floor, Suite 15E,
Off Magadi Road, Ongata Rongai |Tel: +254202319748 |
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website:www.schoolsnetkenya.com

GATUZI LA MAKUENI

JARIBIO LA MTIHANI WA MWIGO

DARASA LA NANE - MWAKA 2016

KISWAHILI

Muda: Saa 1 Dakika 40

SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa karatasi hii ya maswali na karatasi ya kujibia. Karatasi hii ina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika karatasi hii
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika KARATASI YA MAJIBU na wala siyo katika karatasi hii ya maswali.

JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo umeandika katika karatasi ya majibu:

   NAMBA YAKO YA MTIHANI

   JINA LAKO

   JINA LA SHULE YAKO
6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
9. Kwa kila swali 1 - 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

Mfano:

Katika karatasi ya maswali:

17. Mtoto akililia wembe
    A. weka
    B. mpige
    C. mpe
    D. cheza maana

Jibu sahihi ni C. (ufu)

Katika karatasi ya majibu:

16. [A] [B] [C] [D] 17. [A] [B] [C] [D] 18. [A] [B] [C] [D] 19. [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 19. Kisanduku chenye herufi C ndicho kilichorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne vilivyopewa.

Karatasi hii ya maswali ina kurasa 4 zilizopigwa chapa.

FUNGUA UKURASA

Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa

Naikumbuka siku hiyo vyema, ama kweli __1__ niliamka __2__ tayari kuanza safari kutoka __3__ hadi mji mkuu. Hii __4__ iliyokuwa mara yangu ya kwanza __5__ mjini huu. Moyoni nilikuwa na bahasha __6__ va kawaida kwa sababu siku hiyo __7__ mji ambao sifa zake nilikuwa nikisikia kutoka kwa wenzangu waliobahatika kuutembelea. Hamu ya kuona __8__ marefu, barabara __9__, magari mengi, watu wa asili mbalimbali na __10__ starehe ilinigubika kikawa sijifai __11__ matumaini.

1. A. A. siku njema huonekana asubuhi
   B. siku njema uonekana asubuhi
   C. siku njema huonekana asubui
   D. siku njema huonekana alfajiri
2. A. mafungia nyama B. mafungulia ng'ombe C. machwao D. alfajiri mbichi
3. A. kijiji B. kijijini C. mji D. nchi
4. A. ndiyo B. ndio C. ndiye D. ndilo
5. A. kuzuru B. kusuru C. kuudhuru D. kuuzuru
6. A. iliyokuwa B. isiyokuwa C. isiokuwa D. zisizokuwa
7. A. nitauona B. niliona C. ningeliuona D. ningeuona
8. A. jengo B. majengo C. manyumba D. maghorofa
9. A. iliosakifiwa B. silizosakifiwa C. zilizosakifiwa D. ziliosakifiwa
10. A. bustani za B. mabustani ya C. mabaraza ya D. barasa za
11. A. kwa B. na C. ndani D. kwenye

Nilitambaa hatua chache hadi kwenye __12__ cha mabasi, nikapata __13__ moja iliyotoza __14__ nafuu nikaliabiri mpaka mji uliokuwa __15__ kutoka kitongojini mwetu

	A	B	C	D
12.	dugu	stani	kituo	stesheni
13.	daladala	ngalawa	ndege	pantoni
14.	kiingilio	nauli	masurufu	pango
15.	chanda na pete	uta na upote	ulimi na mate	pua na mdomo

Jibu maswali 16 hadi kwa kuzingatia maagizo yaliyotolewa katika kila swali

16. Salamu buriani hutumiwa wakati gani?
   A. Wakati wa matanga
   B. Watu wanaoangana kwa muda mrefu
   C. Mtu aendaposafari ya mbali
   D. Wakati wowote
17. Onyesha kinyume cha
   Wasichana wengi wanaingia darasani haraka
   A. Vijana wachache wanatoka darasani polepole
   B. Wavulana wengi wanatoka darasani polepole
   C. Vijana wachache wanaingia darasani polepole
   D. Wavulana wachache wanatoka darasani polepole
18. Bainisha maneno yaliyopigiwa mstari
   Koboko mnono alitumbukia majini jana
   A. Kielezi, kivumishi, kielezi
   B. Kivumishi, kiwakilishi, kitenzi
   C. Kivumishi, kielezi, kielezi
   D. Kielezi, kielezi, kielezi
19. Kihusishi ni kipi katika sentensi ifuatayo?
   Luvuno alisimama mbele ya hadhira na akatetemeka
   A. alisimama B. mbele ya
   C. hadhira D. akatetemeka
20. Uharibifu uliofanywa hulipwa kwa malipo yaitwayo _____
   A. arbuni B. dia C. fidia D. faini
21. Sukari, chumvi, maziwa ni aina gani za nomino?
   A. Nomino za kawaida
   B. Nomino halisi
   C. Nomino za makundi
   D. Nomino za wingi
22. Joka la mdimu ni kwa mwenye inda ihali _____ ni kwa mwenyewaminifu katika ndoa
   A. Mwenye macho ya nje
   B. Mkono wazi
   C. Mwenye mipango ya nje
   D. Mramba visogo
23. Tambua maana ya sentensi ifuatayo
   Ngomvi angemtii nina yake asingetaabika.
   A. Ngomvi hakumitii nina wala hakutaabika
   B. Ngomvi alimitii nina na alitaambika
   C. ukaidi wa Ngomvi ulimtia matatani
   D. Kutaabika kwa ngomvi kutokana na utiifu wake
24. Tambua matumizi ya 'ki' katika sentensi ifuatayo
   Malii huyo akifika huku atafaa kiafrika
   A. Masharti, kielezi B. Wakati, kielezi
   C. Masharti nomino D. Masharti, hali
25. Ni sayari gani ambayo ina kipenyo kirefu zaidi
   A. Saifeni B. Zohali
   C. Mshatarii D. Mirihi
26. Tegua kitendawili
   Kitu kidogo kimemtoa mfalme kitini
   A. Bunduki B. Kura
   C. Haja ndogo D. Mdudu
27. Mfuko wa ngozi wa kupulizia moto utumiwao na wahunzi huitwa _____
   A. Mvuko B. mvuo
   C. Mfukuto D. Mvuto
28. Je, kaka atamwitaje mume wa dada yake?
   A. Mwanyumba B. Mlamu
   C. Shemeji D. mkoi
29. Shairi la majibizano kati ya watu wawili au zaidi si
   A. uteuzi B. ngonjera
   C. malumbano D. majibazano
30. Kamilisha methali
   Ndege mjanja
   A. halali njaa
   B. hawezi kuwingwa
   C. hunaswa kwa tundu bovu
   D. hukimbiza mbawa zake

Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

Soma kifungu hiki ujibu maswali 21-40

Kunayo imani miongoni mwa jamii nyingi Kenya kwamba wapishi hodari wa ugari hutoka katika maeneo ya magharibi ya Kenya. Ndio maana utazisikia kauli kama vile; "huu ni ugali wa Mkisii au Mluhya". Mpaka leo hii jamii ya Abagusii inasadiki kwamba ndiyo iliyokuwa ya kwanza kabisa kusonga ugali.

Kwa sababu hiyo, moja kati ya kunga nyingi za unyagoni walizofunzwa watoto wa kike kutoka kwa jamii hiyo ni jinsi wangewapikia waume watarajiwa ugali ulioiva. Wavulana kutoka jamii ya Abagusii waliwaambaa wasichana kutoka jamii yao amba hawakuja kupika kwa imani kwamba siku moja wangewaibisha mbele ya wageni hasa wakwe kwa kuwapikia ugali mbichi.

Kimoja kati ya vigezo ambavyo wanaume kutoka jamii hiyo walitumia kumchagua msichana mkamilifu kilikuwa ni kumwomba kuingia jikoni ili kumwandalia mchumba wake na marafiki zake ugali. Kufeli kwenyekenye katika mtihani huo kungekuwa na hatari ya kupigwa buti.

Kwa kuchelea kuachwa na wachumba wao, wasichana Wakisii walijifunga masombo kujifunza kazi za jikoni hususan upishi wa ugali. Ili kuhakikisha kwamba ugali umeiva barabara walimega tonge dogo na kulijaribisha ukutani.

Nitaangazia kisaasili kinachoelezea jinsi jamii ya abagusii ilivyoishia kupika ugali ulioiva' katika masimulizi yangu, nitaazima kutoka katika mojawapo ya kazi za mwandishi mkongwe wa jamii hiyo, Bwongeria. (1960) kisa chenyewe amekipika mada:. Kugingisana kwa wakewenza ndiko kuliufanya ukaiva'. Kinachorejelewa kuwa kiliiva katika muktadha huu ni ugali.

Inasemekana kuwa watu walikula mkorogo wa unga na maji. Mwanaume mmoja kutoka jamii hiyo aliwaoa wanawake wawili ambao hawakuisha kufanyiana fitina au kugingisana. Siku moja, mke wake mmoja alijifungua. Mkemwenza alipewa wajibu wa kumtuza na kumuuguza tumbo la zingizi. Hata hivyo, yule mwanamke alikula njama ya kumwangamiza mwenezake ambaye alikuwa amejifungua.

Badala ya kumpa mkorogo wa unga na maji kama ilivyokuwa mazoea, aliwasha moto akainjika chungu mekoni na baada ya maji kuanza kuchwemka alitia unga na kuanza kusonga mchanganyiko huo. Bada ya kusonga kwa muda mrefu, alimpakulia mkemwenza na kumpelekea ukiwa moto ili aule kwa mtindi au maziwa ya mgando.

Alimtazama akitowelea ugali huo wa mtindi 'Mama mzazi' alipouza kutokwa na jasho kipajini kwa sababu ya joto la ugali, mwenzake alidhani kwamba ule ugali moto umeanza 'kuyatekenya' matumbo yake jinsi alivyopanga. Alikurupuka na kuingia katika nyumba yake. Aliporudi alimkuta mkemwenza amelala fofofo naye akadhani kuwa anakaribia kufariki.

Alirudi tena kwake kwani hakutaka kuhusishwa na mauaji yale. Siku ya pili, alinyatanyata kwenda katika nyumba ya mkemwenza akinyonyesha mtoto, majirani kadhaa wamemtembelea kumwona mtoto aliyezaliwa.

Mwanamke yule alimlimbikizia mwenzake sifa kwa kumpikia chakula kitamu jioni iliyotangulia. Alimwomba ampikie chakula kama hicho wakati wa mchana ili ale na wageni ambao walifurika katika nyumba ile. Wakati wa chamcha, mkemwenza aliyaacha maji yachemke na kufikia kiwango cha mchemko. Kisha, alitia unga na kuanza kuusonga ugali tena.

Mkemwenza na wageni walipoula ugali ule kwa mtindi, walianza kumpalia" mpishi" sifa belele na kumwomba awaoyeshe jinsi ya kupika chakula kama kile. Inaaminika kwamba tangu wakati huo, jamii ya Abagusii ikaanza kupika ugaki ulioiva.

Ni imani ambayo inaonewa fahari kubwa na wanajamii kutokana jamii hiyo. Tofauti na miaka ya awali ambapo vyakula fulani vya kiasili vilikuwa vitambulisho vya jamii fulani, mathalani pure au kande kwa Wagikuyu. muthokoi kwa Wakamba, ugali kwa Abagusii au Abaluhya na nyoyo kwa Waluo, siku hizi mambo yamekuwa tofauti. Jamii yoyote inaweza kupika ugali.

31. Neno kugingisana halina maana sawa na
    A. kukera B. kustawi
    C. kubughudhi D. kuudhi
32. Ni nini maana ya tumbo la zingizi kulingana na kifungu?
    A. Tumbo lililotekenywa na ugali
    B. Tumbo lililotoka moto
    C. Tumbo la 'mama mzazi'
    D. Tumbo la maumivu baada ya kujifungua
33. Chagua jibu sahihi kulingana na kifungu ulichokisoma
    A. Ugali uliopikwa na mama ulidhamiriwa kumwangamiza
    B. Upishi wa ugali mbichi ulichukuliwa kama aibu mbele ya wageni
    C. Zamani vyakula fulani vya kiasili vilikuwa vitambulisho vya jamii fulani
    D. Ugali moto uliopikwa 'mama mzazi'

Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

ulimtekenya matumbo

34. Jamii ya Wabagusii
A. mara ya kwanza waliupika ugali mbichi
B. walivumbua mlo wa ugali
C. waliutowelea ugali kwa mtindi ulioiva
D. Walimpikia 'mama mzazi ugali moto'

35. Mkemwenza alilala fofofo ni fani gani ya lugha?
A. Isitiara
B. Methali
C. Tanakali
D. Tashbihi

36. Chagua jibu lililo na hatua za kupika ugali
A. kuchemsha maji, kusonga, kutia unga, kujaribisha ukutani
B. Kuchemsha maji, kutia unga, kujaribisha ukutani na kusonga
C. Kuchemsha maji, kutia unga, kusonga, kujaribisha ukutani
D. Kujaribisha ukutni, kusionga, kutia unga, kuchemsha maji

37. Kwa mujibu wa kifungu; mkemwenza ni nani?
A. Jibu la mama mzazi katika kifungu
B. Jina linaloitwa mke wa mtoto wako
C. Jina wanaloitana wanawake walioolewa na mume mmoja
D. Jina wanaloitana wanaume waliooa kutoka familia moja

38. Kulingana na kifungu. kisa cha Bwongero(1960) hakielezi
A. Ndoa ya mitara iliyosheheni migogoro
B. Wakewenza waliopendana kama chanda na pete
C. Watu waliokula kikorogo ya unga na maji
D. Mama mzazi aliyepikiwa ugali

39. Unyagoni watoto wa kike hupewa mafunzo ya kunga za kike ilhali watoto wa kiume hupelekwa wapi?
A. Jandoni
B. Kwa nyakonga
C. Kwa kungwi
D. Kwa ngariba

40. Jasho kipajini pa mama mzazi lilisababishwa na nini?
A. Na joto la ugali alioula
B. Na joto la ugali uliopikwa
C. Na kuusonga ugali kwa mda mrefu
D. Na kula ugali kwa mtindi

Soma shairi ulilopewa hapo chini kisha ujibu maswali 41-50;

1. Ndugu zangu **waadhaama**, leo nawaulizia,
Huku pwani na Bungoma, wote mpate sikia,
Wazima hata vilema, **rai** zenu nanuia,
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake **fidia**?

2. Miezi tisa **tamima** tumbo lake nakalia,
Kwa uwezo wa **karima**, mama akajizalia,
Ni mdogo sijasema, shida zangu ajulia,
Kipi cha kumpa mama iwe ni yake **fidia**?

3. Mate kwake nimetema, mama hakunichukia,
Tumbo langu likiuma, kinyesi namtupia,
Chakula hakuninyima, na dawa ya malaria,
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia?

4. Ni mtu mwenye huruma, tena wa kuvumilia,
Hasa uwe ni **vatima**, baba amejifilia,
Akufanyia huruma, **mradi** kutimizia,
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia?

5. Japo nimpe heshima, sioni kama murua
Wema wake nikipima, mbali bado huzidia
Kanipa nyingi huduma, nini nitamlipia?
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia

6. Nikimpa **darahima**, naona sijatimia.
Unga viazi na nyama, sioni kama fidia,
Zawadi zote kupima, ya kumpa sijajua.
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia?

7. Kwa heshima yake mama, kwaheri nawapungia
Naondoka hima hima, swali langu nawachia.
Nenda keti huko nyuma, jibu lenu nangonjea,
Kipi cha kumpa mama, iwe ni yake fidia?

41. Shairi ulilosoma ni la bahari gani?
A. Ngonjera
B. Tathlitha
C. Utenzi
D. Tarbia

42. Wazo la malenga katika ubeti wa tatu ni
A. Mama haogopi kuchafuliwa
B. Mama alimfaa nyakati za taabu
C Mama huhurumia kila mtu
D Mama ana moyo safi

43. Upi ni utao wa mtoto katika ubeti wa tano
A Mbali bado huzidia
B. Wema wake nikipima
C. Nini nitamlipia
D Kanipa nyingi huduma

44. Mtunzi na mwimbaji wa shairi ni _____
A manju
B. mghani
C. malenga
D. Ng.i

45. Sifa zifuatazo zinamjiziwa mama ila
A. mvumilivu
B. mwenye Huruma
C karimu
D. mheshimiwa

46. Kipi cha kumpa mama, iwe yake fidia ni;
A. Kiishio
B. kipokeo
C. kimalizio
D. kituo

47. Silabi ma, ma, ma katika beti zote huitwa _____
A. mizani
B. silabi sahili
C. vina vya kati
D. vina

48. Kanuni zinazotumiwa na malenga kutunga mashairi huitwa _____
A. manthawi
B. muwala
C. inkisari
D. arudhi

49. Swali kuu la mwandishi ni gani?
A. Zawadi bora zaidi kwa mama
B. Malipo mazuri zaidi kwa mama
C. Cha kufidia wema wa mama
D. Fidia bora kwa mama

50. Chagua mada mwafaka kwa shairi hili
A. nimpe nini mama
B. Asante mama
C. mazuri ya nyuma
D. unyumilivu wa mama

Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27